**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**


**MKOA WA NJOMBE**
Anuani **"Afya"**
Nambari ya Simu +25526-2782912
Fax Na. +225 – 262782914
Email:njomberrh@afya.go.tz
**Unapojibu Tafadhali taja:**
Kumb.Na.NJBRRH/APP/01E/15

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,
14 Br. ya Hospitali ya Rufaa,
59107 Ramadhani-Njombe,
S. L. P 1044,
**NJOMBE.**


20 Machi, 2023

Wananchi wote,
**TANZANIA.**

**KUH: TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA WA MUDA MFUPI.**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe kupitia Wizara ya Afya inatangaza nafasi za kujitolea miezi Sita (6) kwa kada zifuatazo;-

**MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA II NAFASI NNE (4)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

a) Kuajiriwa wenye Stashahada NTA Level 6 ya kawaida ya kumbukumbu katika fani ya Afya kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali wenye ujuzi wa kompyuta.

**KAZI NA MAJUKUMU**

(i) Kupokea na kusajili wagonjwa
(ii) Kutunza kumbukumbu za wagonjwa na magonjwa
(iii) Kutafuta na kusambaza mafaili na kumbukumbu za wagonjwa
(iv) Kukusanya, kukagua na kuhifadhi taarifa mbalimbali kutoka wodini.

**MTEKINOLOJIA DAWA II "PHARMACY TECHNICIAN" NAFASI NNE (4)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia Dawa kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

(i) Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.

(ii) Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi

(iii) Kuchanganya dawa

(iv) Kuhifadhi dawa na vifaa tiba

(v) Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa

(vi) Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi katika eneo lake la kazi

(vii) Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa.

(viii) Kuratibu kazi za kamati ya dawa ya hospitali

(ix) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba

(x) Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi

(xi) Kufanya kaguzi mbalimbali katika sehemu zinazohifadhi dawa.

(xii) Kusimamia utendaji wa kazi watumishi walio chnini yake

(xiii) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba

(xiv) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**MASHARTI YA JUMLA.**

1. Ngazi ya mshahara ya kila nafasi itazingatia mwongozo wa kitaifa uliotolewa Julai 2021 unaohusu namna ya kushughulika na malipo ya watumishi wa kujitolea kada za afya au jinsi itakavyoelekezwa na Katibu Mkuu Afya.
2. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi 45
3. Kila mwombaji anatakiwa aambatanishe nakala ya vyeti vya sekondari,taaluma na kuzaliwa na picha ndogo za rangi mbili za hivi karibuni “passport size” pamoja na wasifu binafsi unaoonesha namba za simu na anuani zake na za wadhamini watatu (3) wa uhakika.
4. Waombaji ambao kada zao zinawahitaji wasajiliwe na Bodi zao za taaluma waambatanishe vyeti vya usajiri.
5. Mwombaji aandike nje ya bahasha kada/kazi/nafasi anayoomba
6. Uwasilishwaji wa vyeti vya kugushi utachukuliwa hatua za kisheria.

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Maombi yawasilishwe/kutumwa kabla ya tarehe **28.03.2023** saa tisa kamili alasiri.

Maombi yote yatumwe kwa njia mojawapo kati ya zifautazo;-

1. Kwa mkono; maombi yawasilishwe ofisi ya Masijala Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Njombe siku za kazi.
2. Kwa njia ya barua pepe, muombaji atume "Scanned Documents" kwenda; **njomberrh@afya.go.tz**

barua za maombi zielekezwe kwa **Mganga Mfawidhi** kwa kutumia anuani

**Mganga Mfawidhi,**

**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,**
**14 Br. ya Hospitali ya Rufaa,**
**59107 Ramadhani-Njombe,**
**S. L. P 1044,**
**NJOMBE.**

**NB**: Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe haihitaji mtuma maombi yoyote kutoa fedha katika hatua zote za ajira hii.

Tangazo hili limetolewa tarehe **20/03/2023** na

Hassan M. Haruna
Afisa Mawasiliano
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa
**NJOMBE.**